



**Kanton Bern**  
**Canton de Berne**

# Chekechea katika mkoa unaongea kijerumani wa kanton Bern Haberi kwa wazizi

Elterninformation Kindergarten Suaheli

**Bildungs- und Kulturdirektion**

## **Yaliyomo**

Wazazi wapendwa .....	3
Karibu katika chekecha .....	4
Malengo ya masomo na mbinu za kupeana amri.....	6
Kusaidia maendoleo .....	8
Ushirikiano baina ya wazazi na walimu .....	10
Mpangilio wa chechea .....	12
Utunzaji wa watoto na afya .....	14
Mkuu wa shule, uongozi na huduma maalum .....	15

## **Impressum**

### **Herausgeberin und Copyright:**

Bildungs- und Kulturdirektion  
Amt für Kindergarten, Volksschule und Beratung  
akvb.bkd@be.ch  
Auflage 2022

Download: [www.be.ch/volksschule](http://www.be.ch/volksschule)

## Wazazi wapendwa,

Sasa vile mtoto wako amehitimu miaka minne, kusajiliwa kujiunga na shule ya chekechea katika mwezi wa nane. Kumsajili mtoto wako katika shule ya chekechea ni tukio la maalum sio tu kwa mtoto wako lakini kwako pia. Inamaanisha mwanao atajiunga na kikundi kikubwa cha watoto na itaashiria mwanzo wa miaka kumi na moja ya masomo ya kilazima.

Ikama mzazi unaweza changia pakubwa katika mafanikio ya mtoto wako na kumsaidia katika kazi yake ya shule kwa kupitia utunzaji na msaada. Mhimize mwanao afanye vitu vingi iwezekananvyo yeye mwenyewe kwa kufanya hivyo huongeza kujiamini kwa mtoto, itahimiza kujitegemea na hufanya mwanzo wa shule ya chekechea na maisha kama mojawapo ya kundi kubwa, rahisi zaidi.

Tumekusanya ujumbe wa muhimu zaidi kwako hapa, ili uweze kupata picha kamili ya kile ambacho wewe na mwanao mnaweza tarajia katika shule ya chekechea.

Tunawatakia wewe na mwanao mwanzo mwema usio na wasiwasi na muda wa kuisimua katika chekechea!

Idara ya elimu.

### Tafahali zingatia

Katika manisipaa zingine, watoto wa chekechea wanafundishwa pamoja na watoto walio katika mwaka wa 1 na wa 2 wa shule ya msingi (vikundi vya umri mchanganyiko) katika sehemu ya siku au siku nzima (Basisstufe au cycle élémentaire)

## **Karibu shule ya chekechea!**

### **Kuingia katika chekechea.**

#### **Eintritt in den Kindergarten**

Kujiunga na shule ya chekechea kutafungua nyanja mpya ya maisha, michezo na uzoefu kwa mtoto wako. Atakutana na kundi la watoto ambao wako katika viwango tofauti vya maendeleo yao, wenye mahitaji tofauti, wenye kuzungumza lugha tofauti na waliotoka katika asili tofauti za kijamii na kitamaduni.

Pamoja watoto hawa watakua jamii moja katika chekechea, ambapo wanaweza cheza pamoja na kusomeshana baina yao wenyewe. katika chekechea mtoto wako atapata fursa ya kujaribu vitu vipya, kufanya jaribio na kujenga. matukio tofauti yanayohusu hisia zote yatamuwezesha mwanao kuendeleza mtazamo wake wa vitu na mahusiano baina ya vitu hivyo.

### **Walimu wa chekechea**

#### **Lehrperson für den Kindergarten**

Darasa ambalo limeundwa na watoto walio na umri kati ya miaka minne na sita, linaongozwa na mwalimu wa chekechea. Kwa kutegemea ukubwa wa darasa na waliyomo, kuna uwezekano kwamba mwalimu wa pili wa chekechea atafundisha pia, au msaidizi wa mwalimu atamsaidia mwalimu wa darasa wakati wa masomo.

Mwalimu anamshawishi na kumsaidizi kila mtoto mmoja binafsi kulingana na uwezo wake, maslahi yake na kiwango chake cha maendeleo. Kudhihirika kwake. Mwalimu huyu hutoa msukumo na huchagua njia mwafaka za kutoa amri, hupanga shughuli za kila siku, na hutayarisha vifaa vya masomo ambavyo vinakuza uzoefu upya na maendeleo ya kimasomo.

katika chekechea mtoto wako  
atapata fursa ya kujaribu vitu  
vipya, kufanya jaribio na kujenga.  
matukio tofauti yanayohusu hisia  
zote yatamuwezesha mwanao  
kuendeleza mtazamo wake wa vitu  
na mahusiano baina ya vitu hivyo.

## **Lengo la elimu na mbinu za masharti**

### **Lehrplan 21**

Kufundisha katika chekechea kunategemea Lehrplan. Lehrplan inatumika kama dira inayowasaidia kupanga masomo yao kutoka chekechea hadi mwaka wa 9 wa shule.

### **Kucheza na kusoma**

#### **Spielen und Lernen**

Kucheza ndio njia moja muhimu ya kusoma katika shule ya chekechea. Kucheza kunawakubalia watoto kugundua na kufwata njia zao za elimu. kucheza pia kunakuza uvumilivu wa watoto na kunawapatia motisha ya kujaribu na kusoma zaidi kuhusu kitu na kunawapatia vizingiti mwafaka na fursa za utendaji.

Darasa la chekechea limepambwa na anuwai ya mpangilio wa kucheza na kusoma na mtoto wako atakuwa huru kuamua ni kipi kinampendeza siku yoyote. Watoto wanahimizwa kujaribu njia mpya za michezo na kusoma ambazo hawangechagua wenyewe

Kwa kuanza na masomo yanayoendeshwa na mvuto wa kibinafsi ya kawaida ya kutokana na hali ya maisha ya kila siku na hali ya mchezo, masomo yatakuwa ya mpangilio zaidi wakati ambapo mtoto wako ataendelea na masomo ya chekechea. Uwezo wa mtoto kukabiliana na mazoezi yaliyoandaliwa awali na majukumu utakua muda unavyosonga.

### **Kujifunza kutoka Kwa mwenziwe**

#### **Voneinander Lernen**

Kama mojawapo katika kikundi, mtoto wako atasoma nao na kutoka kwa watoto wengine. Watoto wanasoma kwamba amri ni amri. wanasoma jinsi ya kujibeba vizuri katika hali tofauti na jinsi ya kuambatisha vinavyowavutia na vile vya watoto wengine. Wanajifundisha kujizuia na kujiamini kibinafsi na wanajaribu kupata suluhisho katika hali ya makabaliano. Hii inakuuza maendeleo yao ya ujuzi wao wa utangamano.

## **Kukua kibinafsi**

### **Persönliche Entwicklung**

Watoto pia wanaendeleza ujuzi wao wa kibinafsi katika chekechea. Wanaongozwa kujitegemea zaidi kugawanya majukumu na kuwa watu wenye kuchukua hatua kibinafsi. Kama matokeo kujitegemea kwao kunaongezeka. Wanasoma kulenga malengo yao na kudhibiti hisia zao. Wanajifundisha kujua hisia zao na kujibeba katika hali flani ipasavyo. Watoto wanaendeleza kujiamini kwao na uwezo wao na kutathmini.

## **Viundo msingi vya kupata ujuzi wa kimsingi**

### **Grundlagen für den Erwerb der Kulturtechniken**

Watoto wanajifunza jinsi ya kueleza mawazo yao na hisia zao, kuhusisha matukio na kuskiza hadithi. Hii inakuza ujuzi wao wa lugha na msamiati wao.

Kusikiza silabi na maneno kwenye nyimbo na mashairi huwa andaa watoto kujifunza kusoma na kuandika. Ujuzi wao wa kusonga na uwezo wa kuona nafasi na maumbo pia unaendelea kukua.

Watoto huweza kutambua mahusiano ya hisabati na kanuni katika muktadha wa mwingiliano wa kucheza na idadi na nambari.

**Watoto pia wanaendeleza ujuzi wao wa kibinafsi katika chekechea. Wanaongozwa kujitegemea zaidi kugawanya majukumu na kuwa watu wenye kuchukua hatua kibinafsi.**

## **Kukuza maendeleo**

### **Kukuza na Kuendeleza**

#### **Unterstützen und fördern**

Watoto huleta mahitaji tofauti, uzoefu na ujuzi tofauti katika chekechea. Mwalimu atapima uwezo wa kukuwa wa kiakili wa kila mtoto kwa kuchunguza na kwa kuzungumza na wazazi wake. Hii inamuezesha mwalimu kutambua nguvu za mtoto, talanta na yanayomvutia kutambua ni yapi bado ni magumu kwake. Mwalimu kisha anatumia maono haya ya uzoefu na maendeleo binafsi ya watoto na kupanga kazi yake pamoja na watoto.

### **Usaidizi zaidi**

#### **Zusätzliche Unterstützung**

Watoto ambao wanahitaji usaidizi zaidi kwa maendeleo yao hupokea usaidizi unaowalenga na msukumo unaochochea maendeleo kwa mfano kwa ruhusa yako, mtaalam zaidi anaweza kufanya kazi na mtoto wako kukuza lugha au maendeleo ya kusonga.

### **Kijerumani kama lugha ya pili**

#### **Deutsch als Zweitsprache (DaZ)**

Watoto ambao lugha yao ya asili sio Kijerumani hukuja chekechea na utajiri wa uzoefu na msamiati unaohusika na lugha yao ya kwanza. Kuna raslimali zinazopatikana katika chekechea ambazo hasa zinazolegwa kuwasaidia watoto ambao wanakuwa na lugha zingine kusoma kijerumani.

Mwanao atakuwa na mwanzo mwepesi zaidi kwenye chekechea, iwapo, tayari anaelewa lugha inayotumika kufundisha kupeana masharti na anaweza eleweka na mwalimu na wanafunzi wengine kuanzia mwanzo. Kulingana na mapema kiasi gani mtoto atakutana na lugha ya kijerumani ndivyo itakuwa na wepesi kwake kuisoma. Mtoto wako anapaswa kupewa fursa agalau mwaka mmoja kabla ya kuingia shule ya chekechea. Anapaswa kujifunza akiwa kiwanjani kwa mfano katika hifadhi ya watoto ama akiwa na watoto wengine majirani.



Mwalimu kisha anatumia maono  
haya ya uzoefu na maendeleo  
binafsi ya watoto na kupanga kazi  
yake pamoja na watoto.

## Ushirikiano baina ya wazazi na walimu

### Ushirikiano

#### Zusammenarbeit

Ushirikiano wa mwalimu na mwalimu mkuu kuendeleza mtoto wako kupewa ukuzi mwema na pia ni wajibu wa kisheria wa wazazi.

### Mwafaka kwa shule ya chekechea.

#### Fit für den Kindergarten

Walimu wa chekechea huwasiliana na wazazi mwanzoni mwa mwaka wa shule.

Kuweza kujua chekechea na kukutana na mwalimu siku ya kuzuru shule inaweza ikamsaidia mtoto wako kukuza hisia ya usalama katika mazingira haya mapya.

Utapata mapendekezo ya jinsi ya kumsaidia mtoto wako kukua na kile ambacho kitamuezesha kuwa na mwanzo mwema katika chekechea katika brosha ya 'fit for kindergarden' au kwa: [www.be.ch/fit-fuer-den-kindergarten](http://www.be.ch/fit-fuer-den-kindergarten).

### Habari kwa pande zote

#### Gegenseitige Information

Matarajio na malengo yanaweza fafanuliwa kwa kupitia kubadilishana habari kwa pande zote mara kwa mara na kwa majadiliano. Watoto huwa na tabia tofauti shuleni kuliko nyumbani. Wazazi na walimu wanabadilishana maoni na matukio yao kwa lengo la kumuelewa vyema mtoto na kwa hivyo kumpatia msaada na kumtia moyo.

Mwalimu atakuarifu kwa haraka na mara kwa mara kuhusu kinachofanyika katika chekechea.

Shule ya chekechea itakusadia kwa kumlea na kwenye masomo ya mwanao. Ukihitaji ujumbe wowote au una swali lolote kuhusu shule ya chekechea au kuhusu maendeleo ya mwanao, tafadhali wasiliana na mwalimu wa darasa la mtoto wako.

### **Mbinu tofauti za ushirikiano**

#### **Verschiedene Formen der Zusammenarbeit**

Mwalimu vile vile anaweza akaamua kuhusu mbinu tofauti za ushirikiano na wazazi (kama vile; jioni za wazazi, barua kwa wazazi, majadiliano, hafla za wazazi na watoto).

Hafla katika shule ya chekechea itawapatia fursa wazazi na walimu kuweza kujuana vyema na kukuza uaminifu baina yao.

### **Vikao vya majadiliano**

#### **Gespräche**

Kikao cha majadiliano ili kubadilishana ujumbe na mawazo au kufafanua mambo yoyote unaweza ukaraiwa na mwalimu au mzazi.

### **Mkutano wa mwalimu na mzazi**

#### **Standortgespräch**

Mara moja katika kila mwaka walimu huandaa mkutano wa mwalimu na wazazi. Katika mkutano huu walimu na wazazi hujadiliana maoni yao na kuzungumzia maendeleo ya mtoto, kukua kimasoma ,tabia ya kazi na vile vile ujuzi wa kibinafsi na wa utangamano.

Mwalimu atanukuu majadiliano ya mkutano katika fomu iliyooleanwa na wizara ya elimu kwa shughuli hii(wakiweka sahihi kwa orodha ya mada ) ujumbe zaidi au makubaliano yaliyoafikiwa baina ya walimu na wazazi yanaweza pia yakanukuliwa katika fomu hiyo. Fomu hiyo pia ni baadhi ya folda itakayo kuwa na ripoti ya tathmini ya mtoto wako siku moja.

### **Ziara**

#### **Besuche**

Ziara ya mzazi kwenye chekechea inakubalika iwapo itakuwa baada ya makubaliano na mwalimu.

**Matarajio na malengo yanaweza  
fafanuliwa kwa kupitia kubadilishana  
habari kwa pande zote mara kwa mara  
na kwa majadiliano.**

## Mpangilio wa shule ya chekechea

### Chekechea kama baadhi ya shule ya kilazima

#### Kindergarten als Teil der Volksschule

Chekechea ni sehemu ya kipekee ya shule ya kilazima, ambayo ni ya bure na inaenda kwa muda wa miaka kumi na mmoja. Kama amri chekechea huenda kwa miaka miwili. Kila mtoto akihitimu miaka minne kamili au kabla ya kataruhe 31 Julai ataingia chekechea mwezi Agosti wa mwaka ujayo. Umri ndio unaoamua kusajiliwa.

Wazazi wana wanaweza changua kusubiri mwaka mmoja kabla ya kumsajili mtoto katika shule ya chekechea kwa sababu ya kiwango cha maendeleo cha mtoto. Iwapo unahitaji kuchukua chaguo hilo, tafadhali nakili hilo katika fomu ya kujisaili utakayopewa na serikali ya mtaa wako. Ukitaka unaweza ukatafuta wasia kutoka kwa mwalimu mkuu wa shule kabla ya kufanya uamuzi. Vile vile unaweza tafuta mawaidha kutoka kwa ofisi ya mawaidha ya elimu, daktari wa malezi ya watoto au huduma za mawaidha ya wazazi.

### Masaa ya chekechea

#### Kindergartenzeit

Idadi ya masomo katika chekechea ni (dakika 45) kwa wiki inategemea idadi ya wiki za shule kwa mwaka katika eneo lako la makaazi. Mfano, iwapo kuna wiki 38 za shule, masoma yatakuwa kati ya 23 na 26 kwa wiki, Iwapo kuna wiki 39 za shule masomo yatakuwa kati ya 22 na 25 kwa wiki.

### Kupunguzwa kwa muda wa masomo katika mwaka wa kwanza wa chekechea.

#### Reduktion der Unterrichtszeit im ersten Kindergartenjahr

Katika mwaka wa kwanza wa chekechea wa mwanao, unaweza punguza idadi ya masaa ambayo mwanao anahudhuria chekechea. Tafadhali muarifu mwalimu mkuu kuhusu nua zako wakati wa kujisajili. Muda wa masomo huwezi ukapunguzwa zaidi ya theluthi. chaguo hili limeundwa ili kumwezesha mtoto wako kujumuika katika muda wa masomo mazima pole pole.

Mwalimu mkuu ndiye anayeamua kuhusu mpangilio na muda haswaa wa wakati masomo yaliyopunguzwa.

### Kuhudhuria chekecheo

#### Besuch des Unterrichts

Watoto huudhuria chekecheo mara kwa mara kuanzia jumatatu mpaka ijumaa kulingana na jadwali lililo lililitlewa. Masharti ya chekechea huanza na kuisha katika mda sawa asubuhi kama (wakati wa "block") wa shule. Mafundisho pia hufanyika wakati wa alasiri mara moja au mbili kwa wiki.

Hakikisha mtoto wako anahudhuria masomo akiwa amepumzika ya kutosha. Hakikisha mtoto wako amevaa ipasavyo na amebeba vitu vinavyo hitajika katika mafundisho pia kwa matukio spesheli au matembezi.

## **Njia ya kuenda na kutoka shuleni chekechea**

### **Kindergartenweg**

Wazazi wana jukumu la watoto wao nje ya masaa ya chekechea wakielekea na wanapotoka shuleni. Msaidie mwanao ajue njia ya kuelekea na ya kutoka chekechea ili aweze kujipeleka mwenyewe siku zijazo.

## **Kutohudhuria**

### **Absenzen**

Tafadhali muarifu mwalimu kuhusu kutohudhuria kwa kupangwa (kwa mfano kwa sababu kama vile ugonjwa au ajali inayomuathiri mtoto kwenye familia, kuhama, au muda na daktari au daktari wa meno) kwa muda mwafaka lakini kabla ya somo kuanza. Iwapo mtoto wako ni mgojwa (mfano ana joto mwilini au anahisi kichefuchefu) anapaswa aketi nyumbani hadi atakapo hisi vyema.

## **Kuithinishwa kwa ruhusa ya kutohudhuria kuliopangwa**

### **Dispensationen**

Ruhusa ya kutohudhuria kuliopangwa inaweza ithinishwa tu iwapo ombi la kutohudhuria litawasilishwa kwa mwalimu mkuu wiki nne awali. Ruhusa inaweza kubaliwa kwa sababu zifwatazo; kusheherekea karamu ya maana sana ya kidini, hafla muhimu ya kifamilia, kuhudhuria somo la kujifunza lugha ya mama na tamaduni (HSK).

## **Siku nusu za bure**

### **Freie Halbtage**

Mwanao ana haki ya kuwa na siku tano nusu za bure katika kila mwaka mmoja wa shule. Anaweza akakosa kuhudhuria siku hizi bila kupeana sababu. Unapaswa kumuarifu mwalimu wa darasa awali iwapo unapanga mtoto wako kuomba siku moja nusu ya kukosa kuhudhuria. siku hizo nusu zinaweza chukuliwa moja kwa moja au kwa ujumla.

## **Kuingia katika mwaka wa kwanza wa shule ya msingi**

### **Übertritt in das 1. Schuljahr der Primarstufe**

Kama sheria, kila mtoto huanza shule ya msingi baada ya kumaliza miaka miwili katika shule ya chekechea. Katika kesi maalum –haswa kwa sababu ya kiwango cha maendeleo ya mtoto-anawaeza akaanza mwaka wa kwanza wa shule ya msingi mwaka mmoja mapema ua mwaka moja baadae. Katika kesi hizi uamuzi huu hufanywa na mwalimu mkuu wa shule baada ya ombi la mwalimu wa darasa na kwa kushauriana na wazazi.

Mwalimu wa chekechea na wa darasa la kwanza hufanya kazi pamoja. Miradi ya pamoja na siku ya kuzuru huwapatia fursa ya kujitayarisha kwa kujitayarisha kwa shule ya msingi na kurahisisha mpito.

## Utunzaji wa watoto na afya

### Shule ya kutwa

#### Tagesschule

Shule kadhaa hutoa huduma za 'shule ya kutwa'. (Tagesschulen: programu za kutwa za utunzaji wa watoto alasiri) ambazo zinaweza kuwa nyongeza ya chekechea. Hizi hutoa mwongozo wakati wa mchana (na chakula cha mchana) na wakati wa alasiri shule ya chekechea inapo tamatika. Kuhudhuria kwa shule ya kutwa ni kwa kujitolea. Wazazi huchangia kwa gharama ya Mwongozo na chakula kulingana na mapato yao.

Mkuu wa kila shule anaweza kueleza ni kipi haswaa huendelea huko. Ujumbe wa kijumla kuhusu shule za kutwa unaweza patikana:

[www.be.ch/schulergaenzende-angebote](http://www.be.ch/schulergaenzende-angebote)

Uwezekano zaidi wa utunzaji wa watoto na mwongozo nje ya familia (kituo cha mchana utunzaji wa Watoto, na wataalam wa utunzaji na kadhalika) unapatikana:

[www.fambe.sites.be.ch](http://www.fambe.sites.be.ch)

### Kipimo cha afya

#### Ärztliche Untersuchung

Kipimo cha afya na ukaguzi wa meno na kila mwaka uliofanywa na mtaalam wa meno ni lazima na ni wa bila malipo kwa watoto wote wa chekechea.

Daktari atakarifu iwapo kuna matibabu yoyote yanahitajika. Wazazi wana jukumu la kulipia matibabu kama hayo.

## Mkuu wa shule, ungozi na huduma maalum

### Mkuu wa shule

#### Schulleitung

Mkuu wa shule ana jukumu la kuendesha masomo na mpangilio wa shule na chekechea. Iwapo una swali kuhusu swala la mpangilio wa shule au hali ambayo haiwezi tatuliwa na mwalimu, unaweza jadili swala hilo na mkuu wa shule.

### Serikali ya mitaa

#### Gemeindebehörde

Serikali ya mitaa inalo jukumu la kuhakikisha watoto wanahudhuria shule ya chekechea kulingana na sheria ya kantoni na amri za mitaa.

### Mkaguzi wa shule

#### Schulinspektorat

Mkaguzi wa mitaa wa shule anasimamia masomo ya kilazima katika kantoni.

### Ofisi ya elimu ya ushauri

#### Erziehungsberatungsstellen (EB)

Ofisi ya elimu ya ushauri katika mkoa wako inaweza kupatia wasia katika maswala yako kuhusiana na maendeleo ya mtoto wako na maswali maalum ya elimu:

[www.be.ch/erziehungsberatung](http://www.be.ch/erziehungsberatung)

Ujumbe zaidi kuhusu masomo ya kilazima yanaweza patikana:

[www.be.ch/volksschule](http://www.be.ch/volksschule)

